

Tumtolee Mungu wetu

Musique de François TUTU MAKANGA

♩ = 70

1. Ndu-gu za-ngu tu-so-ge-e Tu-mto-le-e Mu-ngu we - tu. Twe-nde kwa-ke
na sa-da ka

tu. Yo-te tu-me - pe-wa na-ye Hi-vyo vyo-te ma-li ya - ke. Ku-mbe tu-to ke.
we kwa mo-yo. Hi-vyo vyo-te ma-li ya ke.

1. Ndugu zangu tusogee: TUMTOLEE MUNGU WETU WETU

Twende kwake na sadaka: TUMTOLEE....
Yote tumepewa naye: HIVYO VYOTE MALI YAKE;
Kumbe tutoe kwa moyo: HIVYO ...

5. Mazao ya kazi zetu: TUMTOLEE MUNGU

Na pesa za mifukoni: TUMTOLEE
Tuzipeleke kwa Bwana: HIVYO VYOTE M...
Ili tupate baraka : HIVYO ...

2. Tupeleke mali zetu : TUMTOLEE

Tulizo zipata kwake : TUMTOLEE ...
Tumtolee na furaha : HIVYO VYOTE ...
Tusiwe na choyo kwake : HIVYO VYOTE ...

6. Na wanyama wa mifugo : TUMTOLEE ...

Maisha, elimu yetu : TUMPTOLEE ...
Kwa kuwa vyote ni vyake : HIVYO VYOTE
Rudisha shukrani kwake : HIVYO VYOTE ...

3. Tutoe shukrani zetu: TUMTOLEE

Kwa yale atudjalia : TUMTOLEE ...
Tujue ya kwamba vyote : HIVYO VYOTE ...
Tutoe kwa ukarimu : HIVYO VYOTE

7. Manemane na uvumba : TUMTOLEE

Mukate nayo divai : TUMTOLEE ...
Sadaka iliyo safi : HIVYO VYOTE ...
Yatupatanisha wote : HIVYO VYOTE

4. Sawa na yule mujane : TUMTOLEE

Katoa aliyo nayo : TUMTOLEE ...
Tufanane na mujane : HIVYO VYOTE ...
Ndivyo tutabarikiwa : HIVYO VYOTE

8. Sifa kwako Mungu Baba : TUMTOLEE

Kutudjaza naye Mwana : TUMTOLEE ...
Roho katupa mapendo : HIVYO VYOTE ...
Tuishi milele yote : HIVYO VYOTE ...